## HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA JUMANNE TAREHE 26/10/2021 SAA 2.00 ASUBUHI KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO MANISPAA YA KIGAMBONI MUHT.03/2021-2022

MAHUDHURIO

1. Wenceslaus Lindi - Mwenyekiti
2. Godfrey Mwangairo - Katibu
3. Happy Luteganya - Mjumbe
4. Pius G.Mutechura - Mjumbe
5. Priscilla Mhina - Mjumbe

MWALIKWA

1. Charles P.Lawisso - Mwanasheria wa Manispaa

SEKRETARIETI

1. Henry Rugayi - Afisa Ugavi II
2. Leah Semwenda - Afisa Ugavi II

Agenda

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kupitia taarifa ya Uchambuzi kwa ajili ya kumpata fundi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wenye kifua kikuu (MDR – TB) katika hospitali ya vijibweni
4. Kupitia taarifa ya mafundi wa kujenga madarasa katika shule za sekondari za Minazini,kimbiji,kisarawe II,Aboud Jumbe,kidete,pembamnazi na somangila na shule shikizi za Golani kimbiji na kwa Moris pamoja na ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye uhitaji maalum katika shule ya msingi Chekeni Mwasonga kwa kutumia fedha za COVID - 19
5. Kufunga kikao

**Agenda 1 MUHT.03/2021-2022 kufungua kikao**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwapa taarifa kuwa tumeitana hapa kwa dharura hivyo kikao cha leo kitakuwa na agenda mbili tu ambazo tutaelezwa na katibu wa kikao chetu baada ya hapo aliwaomba wajumbe wajadili agenda zilizo mbele yao kwa Manufaa ya Halmashauri yetu kisha alifungua kikao saa 2.05 Asubuhi.

**Agenda 2 MUHT.03/2021-2022 kuthibitisha agenda**

Mwenyekiti aliwauliza wajumbe kama kuna agenda ya Nyongeza, wajumbe walithibitisha agenda kama zlivyowasilishwa

**Agenda 3 MUHT.03/2021-2022 Kupitia taarifa ya Uchambuzi kwa ajili ya kumpata fundi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wenye kifua kikuu (MDR – TB) katika hospitali ya vijibweni**

Katibu alitoa taarifa kuwa kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kimepokea taarifa ya uchambuzi kutoka kwenye kamati ya tathmini kwa ajili ya kumtafuta fundi wa kujenga jengo la wagonjwa wenye kifua kikuu sugu linalotarajia kujengwa katika hospitali ya vijibweni.Katibu aliendelea kueleza kuwa taarifa hiyo ya tathmini pia imewasilishwa katika kikao hiki cha dharura na wajumbe wote mnayo pia muipitie kwa makini ili kuweza kutoa maamuzi sahihi.Aidha kwa upande wa kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kimepitia taarifa hii kwa makini na kimerizika kuwa uchambuzi umefanywa kwa kufuata sharia ya ununuzi wa umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 pia kanunuzi za ununuzi wa umma za serikali za mitaa za mwaka 2018 ,kitengo kinakubaliana na mapendekezo ya timu ya tathmini kuwa fundi **Elamu Daniel Mmochi apewe kazi ya ujenzi wa jengo la kifua kikuu katika hospitali ya Vijibweni kwa gharama ya Tshs.137,820,000/- (Miamoja therathini na saba milioni laki nane na ishirini elfu) tu kwa muda wa miezi sita (6)**

Baada ya taarifa ya katibu mwenyekiti alitoa nafasi kwa wajumbe ili waweze kuchangia. Mjumbe mmoja ambaye pia ni Mhandisi wa Manispaa alichangia kuwa ameona gharama za ufundi ziko ndani ya asilimia za mapishano kati ya makadirio ya mhandisi na uhalisia wa mwombaji ambazo ni asilimia 15 juu au chini ya makadirio ya mhandisi,pia alizungumzia swala la muda wa ujenzi kuwa unatosha kwa fundi kumaliza kazi zake lakini pawe na mtiririko mzuri wa upelekaji vifaa site.

Mjumbe mwingine alichangia kuwa yeye anakubaliana na maoni/mapendekezo ya PMU kwani amepitia taarifa ya tathmini ameona iko vizuri. Baada ya majdiliano hayo kukamilika wajumbe kwa wote kwa kauli moja wamempitisha fundi **Mmochi kufanya kazi ya ujenzi wa jengo la kifua kikuu katika hospitali ya Vijibweni kwa gharama ya Tshs.137,820,000/- (Miamoja therathini na saba milioni laki nane na ishirini elfu) tu kwa muda wa miezi sita (6)**

**Agenda 4 MUHT.03/2021-2022 Kupitia taarifa ya mafundi wa kujenga madarasa katika shule za sekondari za Minazini, kimbiji, kisarawe II, Aboud Jumbe, kidete, pembamnazi na somangila na shule shikizi za Golani kimbiji na kwa Moris pamoja na ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye uhitaji maalum katika shule ya msingi Chekeni Mwasonga kwa kutumia fedha za COVID - 19**

Mwenyekiti alimkaribisha katibu kutoa taarifa juu ya agenda hii.Katibu alitoa taarifa kuwa kama mnavyofahamu kwa sasa kuna ujenzi wa madarasa unatakiwa uanze katika manispaa yetu ya kigamboni,ujenzi utafanyika kwa fedha zilizotolewa na serikali kuu chini ya mpango wa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19 ambapo idara ya elimu Msingi imepokea fedha kiasi cha Tshs.80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne (4) na Idara ya elimu sekondari imepokea fedha kiasi cha Tshs.680,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 34.Lakini pia mnafahamu kuwa serikali imetoa maelekezo kwamba ujenzi huu ufanyike kwa utaratibu wa "Force Account" na inakubalika kutumia njia ya "Single source".Aidha imeelekeza/agiza ununuzi wa pamoja (Bulky Procurement) ufanyike kwa baadhi ya vifaa kama vile Nondo,Saruji,Mbao na Mabati

Mkurugenzi kupitia kikao cha menejimenti aliunda timu ya ufuatiliaji kama maelekezo ya viongozi wa ngazi za juu yalivyoelekeza,baada ya kuundwa timu aliitisha kikao cha pamoja kilichowahusisha baadhi ya wakuu wa idara,timu ya ufuatiliaji iliyoteuliwa,wakuu wa shule na walimu wakuu wa shule zenye miradi na watendaji wa kata ili kwa pamoja waamue namna bora ya kutekeleza hii miradi ndani ya kipindi kifupi.Kikao kiliamua pamoja na mambo mengine kupendekeza majina ya mafundi wenye sifa,uwezo na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi wa madarasa haya.Mafundi waliopendekezwa ni kama ifuatavyo hapa chini;-

1. Bandiko Athumani – Atajenga madarasa katika shule ya sekondari Kidete
2. Mpoki Kalyembe - Atajenga madarasa katika shule ya sekondari PembaMnazi
3. Fredrick Bimba - Atajenga madarasa katika shule shikizi ya kwa Morisi
4. Davis Ndosi - Atajenga madarasa katika shule ya sekondari Kimbiji (madarasa 4)
5. Bernard Ngoda - Atajenga madarasa katika shule ya sekondari Kimbiji (madarsa 4) na shule shikizi ya Golani Kimbiji
6. Filbert Ndunguru - Atajenga madarasa katika shule ya sekondari Mizimbini
7. Gasper Haule - Atajenga madarasa katika shule ya sekondaria Aboud Jumbe

8. Shabani Siwa - Atajenga madarasa katika shule ya sekondari Kisarawe II

9. Chesco Nyaulingo - Atajenga madarasa katika shule ya sekondari Somangila

10. Davis Ndosi - Atajenga bweni la wanafunzi wenye uhitaji maalum katika shule ya msingi ya Chekeni Mwasonga

Hivyo PMU inaomba kwenu bodi ya zabuni mambo yafuatayo

I. Mpitishe ujenzi wa madarasa haya pamoja na bweni ufanyike kwa utaratibu wa Force Account

II. Muwapitishe mafundi wote walioorodheshwa hapo juu ili wajenge madarasa na bweni husika

III. Mpitishe Ununuzi wa baadhi ya vifaa ufanyike kwa njia ya pamoja (bulky procurement)

IV. Mpitishe Ununuzi wa vifaa ufanyike kwa utaratibu wa force account ambapo njia za minor value na micro value procurement zifanyike

V. Mpitishe mabadiliko yafanye kwenye mpango wetu wa Ununuzi wa mwaka 2021/2022 ili tuingize na ununuzi huu

**Baada ya taarifa na maombi ya katibu kutolewa,mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kuchangia ambapo wajumbe wote baada ya michango mbalimbali iliyokuwa inafanana waliamua kuwa maombi yote yaliyoombwa na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi yamepitishwa na wajumbe wa bodi ya zabuni**

**Agenda 5 MUHT.03/2021-2022 kufunga kikao**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu na weredi wao walio utumia wakati wote wa kikao na aliwashukuru kwa michango yao mizuri kisha aliahirisha kikao saa 4.45 asubuhi.

**MWENYEKITI** 2/12/2021

**WENCESLAUS LINDI**

**KATIBU** 2/12/2021

**GODFREY MWANGAIRO**